# OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI
# HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA
## SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA MSALATO

**S. L. P. 933, DODOMA. SIMU NA. 0782972370, 0757887948, 0757408486**

Kumb. Na. MG/F/3/VOL.2/F.I

Mpendwa Mwanafunzi:- …………………………………………………….…….. …………………………….

Anwani: c/o ……………………………….(Mzazi/ Mlezi), S. L. P……………………………………………

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA SHULE YA SEKONDARI YA MSALATO KATIKA HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA MWAKA 2026**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha kwanza katika Shule hii mwaka **2026**.

Shule iko kilomita kumi (10km), kaskazini mwa mji wa Dodoma, ukifuata barabara kuu iendayo Kondoa-Arusha. Usafiri wa daladala unapatikana kituo cha daladala cha Machinga panda daladala iendayo Veyula/Msalato shuka kituo cha Bible, nauli ni sh. 700/= kwa pikipiki ni shilingi 10,000/= na kwa bajaji ni shilingi 15,000/= tu, wanaotokea Arusha kuja Dodoma shuka kituo cha Msalato Bible.

Mwisho wa kuripoti ni saa 10:00 jioni. Ukikwama piga simu hiyo hapo juu kwa ushauri na maelekezo zaidi.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe **13.01.2026** hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni ijumaa tarehe **09.01.2026** Mwisho wa kuripoti ni tarehe **23.01.2026** Endapo hutapenda kujiunga na shule hii toa taarifa ya maandishi ndani ya hizo wiki mbili. Hali kadhalika, epuka usumbufu kwa kufika shuleni hapa kwa **nyaraka na jina la mtu mwingine**! Njoo na barua hii kwa utambulisho. Omba kuonana na mwalimu wa zamu ambaye atakupokea na baadae kukuelekeza kwa 'boarding master' wa shule kwa ajili ya kukabidhi vifaa vilivyoelekezwa hapa chini.

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 2.1 a) Sare za Shule

i) Mashati meupe mawili (2) yenye mikono mifupi na mfuko upande wa kushoto.

ii) Sketi za darasani, mbili (2) kitambaa cha suti esteem namba moja (1) **bluu bahari** (light blue) yenye marinda yanayoangalia upande mmoja na yanayolingana kati ya 13 - 15, **na iwe ndefu kufikia kifundo cha miguu (IGUSE KIATU).**

iii) Sketi za nje ya darasa, mbili (2) kitambaa cha suti esteem namba moja (1) **damu ya mzee** (maroon) mshono wa solo ambayo siyo pana sana, **iwe ndefu kufikia kifundo cha miguu** (IGUSE KIATU).

iv) T-sheti 2 vazi la nje ya darasa yenye kola (form six). **Inapatikana shuleni**

v) Sweta 2 nyeusi zenye shingo ya V mbele.

vi) Tai ndefu ya pundamilia rangi ya light blue na dark blue. **Inapatikana shuleni**

**2.1 b) KWA WANAFUNZI WAISLAMU**:

i) Nusu kanzu nyeupe mbili (2) zenye mikono mirefu.
ii) Hijabu mbili nyeupe na vikofia vyeupe kitambaa cha kotoni ndefu yakufunika mikono.
iii) Sketi za darasani, mbili (2) kitambaa cha suti esteem namba moja (1) **bluu bahari** (light blue) yenye marinda yanayoangalia upande mmoja na yanayolingana kati ya 13 - 15, **na iwe ndefu kufikia kifundo cha miguu** (IGUSE KIATU)
iv) Sketi za nje ya darasa, mbili (2) kitambaa cha suti esteem namba moja (1) **damu ya mzee** (maroon) mshono wa solo ambayo siyo pana sana, **iwe ndefu kufikia kifundo cha miguu** (IGUSE KIATU)
v) Hijabu mbili za damu ya mzee (maroon) na vikofia vyake vazi la nje ya darasa kitambaa cha kotoni ndefu yakufunika mikono.
vi) T-sheti 2 vazi la nje ya darasa **RANGI YA KIJIVU** iliyokolea yenye kola (form six) **inapatikana shuleni.**
vii) Sweta 2 nyeusi zenye shingo ya V mbele.

## 2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

a) Daftari kubwa "counter book Q3" jumla 12 au zaidi,kalamu, penseli, rula, mkebe wa Hisabati n.k
b) **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) aina ya "Double A" kwa mwaka;
c) Viatu vya shule vya ngozi nyeusi vya kufunga na kamba jozi 2 (kisicho na kisigino wala si buti), kiwi na brashi yake na **soksi nyeupe ndefu zisiwe na weusi kwenye unyayo angalau jozi 2**. Pia aje na raba nyeupe **siyo buti** jozi moja kwa ajili ya michezo.
d) Track Suit **rangi moja.** Iwe nyeusi au bluu nyeusi (dark blue) yenye mistari mitatu nyeupe pembeni kwa ajili ya mazoezi na kuzuia mbu na baridi anapojisomea usiku.
e) Vifaa vya kulia chakula kama Container, kikombe, kijiko na chombo safi cha kuhifadhia maji ya kunywa.
**f)** Mto, shuka (Pink) 2 na foronya (Pink) 2 na blanketi moja zito. Aje na taulo na jozi moja ya kitenge au khanga, Net (chandarua) ya futi 3 ½ rangi nyeupe, vibanio vya nguo seti moja. **Nguo nyingine haziruhusiwi kabisa.**
**g)** Vifaa vya usafi binafsi kama sabuni, mswaki na dawa, mafuta ya mgando ya kujipaka mwilini, 'always, toilet paper', ndala aina umoja na viatu vya kimasai (Masai culture) vyenye shanga na visifungwe nyuma.
**ZINGATIA- Losheni, Perfume/Spray na mafuta yenye harufu kali haviruhusiwi kabisa.**
h) Nguo za ndani za kutosha kama chupi, shimizi/gagulo, skin tight fupi, sidiria n.k ziwe nyeupe au nyeusi tu.
**i) Nguo za kulalia (night dress) rangi nyeupe au nyeusi, nyepesi zinazoangaza.**
j) Tochi na betri/Taa ndogo ya jua, sanduku imara **trunker** na pia vazi rasmi la shule.
k) Ndoo ya kuogea na kuhifadhia maji lita 10
l) **Ni lazima kila mwanafunzi awe na** Kitambulisho cha Bima ya Afya**. Kama hana atalipia Tsh50,400 ili akatiwe bima.**

**2.3 Godoro**

Godoro futi 2 ½ x 6 lenye upana wa kutosha ataazima Shuleni kwa sh. 10,000/= kwa kila mwaka. Malipo ya kuazima godoro la Shule yalipwe kwenye akaunti namba **50501100161 - NMB**
Jina la akaunti ni **Msalato Secondary Schoo**l lipa **popote ulipo hapa nchini.** Kabidhi stakakabadhi ya benki yenye **jina la mwanafunzi** kwa "boarding Master" mara tu ufikapo shuleni. **Hatupokei fedha taslim.**

**2.4 VIFAA VYA USAFI**

Mwanafunzi anatakiwa kuja na vifaa vya usafi kama ifuatavyo;-
Mfagio wa nje mgumu (chelewa) wenye mpini na laini wa ndani, Sqeezer 'Moper' kwa ajili ya kudekia chooni na bafuni, sabuni ya maji aina ya Dexi lita tano.

**3.0 ZINGATIA: -** Ni muhimu kuzingatia yafuatayo kumwondolea bughudha binti yako awapo hapa shuleni.

**a) Fedha kwaajili ya Matumizi Binafsi na Nauli:-** Apewe mwanafunzi mkononi. Mzazi akadirie vema matumizi ya binti yake ili asiwe mbadhirifu au mdokozi wa fedha au mali za wenzake. Pia, shule hufungwa mwanzoni mwa miezi Juni na Desemba kila mwaka. Pia mapumziko mafupi April na Septemba. Ni wajibu wa mzazi kufikisha nauli mapema kwa binti yake aweze kurejea nyumbani kipindi cha likizo. ***Mihula ya Shule ni kama ifuatavyo:-***

| ***MIHULA*** | ***Kufungua*** | ***LIKIZO FUPI*** | | ***Kufunga*** | ***IDADI YA SIKU ZA MASOMO*** |
|---|---|---|---|---|---|
| | | ***Kufunga*** | ***Kufungua*** | | |
| *Mhula I* | *13.01.2026* | *27.03.2026* | *08.04.2026* | *05.06.2026* | *96* |
| *Mhula II* | *06.07.2026* | *04.09.2026* | *14.09.2026* | *04.12.2026* | *98* |
| ***Jumla ya Siku za Masomo*** | | | | | ***194*** |

***NB: - Iwapo kutakuwepo na mabadiliko mzazi/mlezi utaarifiwa.***

**6.2 Afya:-** Ni jukumu la mzazi/mlezi kuhakikisha afya ya binti yake. Hivyo, anatakiwa kumpeleka Hospitali ya Wilaya, Mkoa au Rufaa ili akapimwe kikamilifu na kujaziwa fomu iliyoambatishwa. Wazazi wasitumie mazoea kwa kupitia njia za mkato kuwataka waganga kuwajazia fomu hiyo bila kufanyiwa vipimo halisi. Mwenye maradhi ya kudumu aje na barua ya daktari wa Wilaya, Mkoa au Rufaa kuelezea tatizo la mwanafunzi huyo. Aidha mpatie mwanao bima ya afya au fedha ya matibabu, atakapohitajika kutibiwa hospitali za nje kwani shuleni hutolewa huduma ya kwanza tu.

**6.3. Sheria na kanuni muhimu za shule.**

6.3.1 Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni:

a. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu.
c. Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni (preparation)
d. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
e. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
f. Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.
g. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
h. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

**6.3.2. Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha ukafukuzwa shule**:

a. Wizi.
b. Uasherati na ushoga.
c. Ubakaji
d. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya au kukutwa na bangi, cocaine, mirungi, kubeli, sigara n.k.
e. Kupigana au kumpiga mwanafunzi au mtumishi wa shule.
f. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
g. Kudharau Bendera ya Taifa
h. Kuoa au Kuolewa
i. Kupata mimba au kuharibu mimba ndani na nje ya shule.

j. Kulala nje ya shule bila taarifa
k. Kugoma, kuchochea na kuongoza mgomo au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
l. Kutukana watu kwa makusudi.
m. Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi au vitu vinavyohusiana na simu kama vile vocha, chaja, laini ya simu, au earphone .
n. Kukosa shule kwa siku 90 mfululizo bila taarifa rasmi.
o. Kuchelewa kufika shuleni kutoka likizo au unaporuhusiwa kutoka nje ya shule.
p. Utoro (kutoka nje ya mipaka ya shule bila ruhusa)
q .Kugomea maelekezo halali ya shule mfano kazi, chakula, masomo n.k
r. Kulala kitanda kimoja wanafunzi wawili.
s. Mwanafunzi kujihamisha bweni alilopangwa na utawala bila taarifa.

**6.4 Ni marufuku** mwanafunzi kumiliki vifaa vya anasa kama vile Redio, Kompyuta mpakato, Cheni, kufuga kucha au kupaka rangi kucha, kufuga nywele na kusuka au kuweka nywele dawa.

6.5 **Vielelezo**:-

a. Afikapo shuleni, akabidhi kwa MSAJILI (BOARDING MASTER) barua hii, fomu iliyojazwa na daktari na kivuli cha cheti chake cha kuzaliwa au cha uraia kama si Mtanzania.
b. Akabidhi fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi.
c. Mzazi akabidhi fomu ya kukiri kukubaliana na sheria, kanuni, na malelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

Tafadhali soma kwa makini maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu. Ninakutakia Maandalizi na Safari Njema kuja Msalato Sekondari

**KARIBU SANA MSALATO SEKONDARI**

MBMsokola

……………………….

***Mwasiti B.Msokola***

**MKUU WA SHULE**

HEADMISTRESS
P. O. Box 933
DODOMA
MSALATO SECONDARY SCHOOL

# OFISI YA WAZIRI MKUU

***TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA***
***HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA***
***SHULE YA SEKONDARI YA MSALATO***
***S.L.P. 933: SIMU 026 - 230 2666 DODOMA***


## SHERIA ZA SHULE

**UTANGULIZI**
Shule ni mahali pa kuwalea na kuwakuza watoto katika mazingira ya kitanzania ili wanapohitimu masomo yao wawe raia na watumishi bora; walio tayari kujitegemea. Sheria zifuatazo ni lazima zizingatiwe na kufuatwa ili kutekeleza azma hiyo:-

**A: MASOMO**

***1.*** Inamlazimu kila mwanafunzi kuhudhuria vipindi vyote vya masomo; kufanya majaribio, mazoezi, Mitihani na shughuli zote za nje ya darasa kwa wakati uliopangwa na kuwasilisha kunakotakiwa kwa wakati bila visingizio. ***Ifahamike pia kuwa shughuli yoyote nje ya darasa ni sehemu ya malezi ya mtoto yenye lengo la kuboresha taaluma yake.*** Shughuli hizo ni kama miradi ya uzalishaji mali, usafi, mchaka-mchaka, michezo, gwaride, na shughuli nyingine za mikono na ukakamavu.

***2.*** Ni marufuku kupiga kelele, kuzagaazagaa, kuandika barua/nyimbo, kusikiliza muziki/ starehe nyingine, kuandika ubaoni, kutoka nje ya darasa/bweni na kufanya jambo lolote tofauti na tukio husika nje ya utaratibu wa Shule.

***3.*** Mwanafunzi asiingie maabara, ofisi, chumba cha walimu, nyumbani kwa walimu/walezi wala sehemu yeyote bila ruhusa ya mwalimu. Sheria na taratibu za maabara na maktaba ya shule zizingatiwe kikamilifu.

**B: MAVAZI**
Kila mwanafunzi atavaa vazi rasmi la shule wakati wote wa masomo, maandalizi ya mchana, mikutano/tafrija muhimu ya shule, aendapo nje ya shule na pia asafiripo kwenda likizo na kurudi.

Ni marufuku mwanafunzi kuvaa nguo, mavazi na marembo mengine ya nyumbani, kunyoa kipara, kusuka au kufuga nywele, kutumia madawa au kupaka rangi nywele, kucha / midomo. Pia mwanafunzi hatakiwi kuvaa heleni, bangili, pete, mikufu, rozari/tasbihi, hirizi, mikanda na mapambo ya aina yoyote ile akiwa amevaa mavazi ya shule awapo ndani ya shule.

**C: RUHUSA**
***Mipaka ya shule kwa wanafunzi ni maeneo yao ya madarasa/vyumba vya kusomea, mabwenini, viwanja vya michezo na maeneo ya usafi.***

***1.*** Ni marufuku mwanafunzi kutoka nje ya mipaka ya shule bila ruhusa ya uongozi wa shule bila kibali hujisababishia kosa kubwa la utoro.

***2.*** Mwanafunzi haruhusiwi kwenda ofisini au kwenye nyumba za walimu na watumishi wengine isipokuwa patokeapo dharura. Hata hivyo, mwanafunzi ataeleza shida au tatizo mlangoni na kugeuza mara moja. Iwapo mwanafunzi atalazimika kwenda nyumbani kwa mwalimu/watumishi kwa masuala ya kawaida, lazima apate kibali kutoka kwa mwalimu wa zamu; ambaye yeye mwenyewe, *haruhusiwi kumtuma mwanafunzi kwenda nyumbani kwake.*

***3.*** Ni marufuku mwanafunzi kutoka nje ya shule bila kibali cha mwalimu wa malezi endapo ni ruhusa ya kawaida. Kwa wagonjwa, sharti matroni aidhinishe kwanza na Hospitali atakayoenda lazima kibali hicho kigongwe mhuri na kusainiwa na Daktari atakae mtibu. Pia ieleweke kuwa ni kosa kubwa mwanafunzi kutoripoti na kurudisha kibali kwa mwalimu wa zamu arejeapo baada ya kuruhusiwa.

***4.*** Wanafunzi hawatapewa ruhusa kwenda benki, posta, vituo vya mabasi, stesheni au kwa ndugu mjini kufuatilia nauli, vifurushi, mzigo n.k. Wazazi watumie vema huduma za posta au wafike wenyewe shuleni kutoa huduma hizo.

***5.*** Ni marufuku mwanafunzi kulala nje ya shule, kuhudhuria sherehe zozote zile. Kibali cha kulala nje kitatolewa na Mkuu/Kaimu wa Shule endapo mwanafunzi atafiwa na mama, baba mzazi, mlezi pekee, dada au kaka wa tumbo moja. Sherehe na tafrija zitakazohitaji kuwapo mwanafunzi nyumbani zifanyike nyakati za likizo yao.

***6.*** Mara moja moja, Mkuu wa Shule atatoa ruhusa kwa wanafunzi kwenda mjini kwa awamu kubadilisha mazingira. Endapo masharti ya ruhusa hatayazingatiwa, Mkuu wa Shule anaweza kuondoa fursa hiyo kwa wahusika au kwa wanafunzi wote kwa muda usiojulikana.

**D: CHAKULA**

***1.*** Sharti chakula kiliwe *bwaloni kwa wakati* uliopangwa. Ni marufuku kutoa chakula nje ya bwalo, kukipeleka mabwenini au darasani.

***2.*** Ni marufuku kubebeana vyakula. Wagonjwa walale Zahanati ili walioruhusiwa kuwahudumia wawapelekee chakula huko.

***3.*** Ni marufuku wanafunzi kuletewa au kuleta chakula shuleni mbali na kinachopatikana hapa shuleni. Kufanya hivyo kutasababisha wahusika kuchukuliwa hatua za kinidhamu.

***4.*** Ni marufuku kutupa ovyo mabaki ya vyakula, soda, pamoja na taka nyinginezo. Mapipa na mashimo ya taka yatumike kwa kazi hiyo.

**E: AFYA**

***1.*** Kila mwanafunzi anayejiunga na shule hii apimwe na Daktari wa Wilaya/Mkoa/Rufaa kuthibitisha kwamba afya yake inamruhusu kuendelea na masomo. Pia wanafunzi wote watapimwa afya zao na matroni wa shule wakati wowote shule inapoona inafaa. Ni muhimu pia wanafunzi wapate vipimo na matibabu kikamilifu kabla ya kurejea shuleni pindi wanapokuwa likizo.

***2.*** Mwanafunzi aliye na matatizo sugu kama sickle cell, moyo, kifua, macho n.k. aje na vyeti vyenye maelezo kamili ya daktari akionesha tiba sahihi ya mtoto huyo, pamoja na dawa za akiba kwa ajili ya tahadhali. Mwanafunzi wa aina hii atoe taarifa hii kwa matron, mwalimu wake wa bweni/darasa mara tu anapowasili shuleni. Ni marufuku kujitunzia dawa mwenyewe bila idhini ya daktari au matroni wa shule.

***3.*** Ni wajibu wa mwanafunzi anayeumwa kutoa taarifa kwa matron mwalimu wa zamu mara moja. Ni marufuku kucheleweshа kutoa taarifa za ugonjwa kwa vigezo vya kuombewa na kukemea mapepo. Atakayegundulika akishiriki tabia hii atachukuliwa hatua kali sana ya kinidhamu ikiwa ni pamoja na kurejeshwa nyumbani kumleta mzazi/mlezi au kufukuzwa shule kwa kosa la kuhatarisha maisha yake.

***4.*** Mwanafunzi anayeumwa atapata huduma ya kwanza katika zahanati ya shule. Ikishindikana ataagizwa kwenda hospitali ya Mkoa ya Dodoma au Benjamin Mkapa, Makole, Milembe kwa vipimo au matibabu zaidi. Iwapo mwanafunzi atazidiwa wazazi wake wataaarifiwa na **Mkuu wa Shule**. *Taarifa yoyote itakayomfikia mzazi kwa njia tofauti; ni batili na mhusika atawajibishwa kikamilifu.* Ni marufuku mwanafunzi kujichagulia/kukataa matibabu sahihi aliyoshauriwa na dakatari au matroni.

**5.** Ni makosa mwanafunzi mgonjwa kulala bwenini. Wagonjwa wote walale zahanati ya shule kwa kibali cha matroni au mwalimu wa zamu. Pia, muda wa matibabu katika zahanati ya shule uzingatiwe kikamilifu.

**F: UTUNZAJI WA MALI**

*Ni marufuku kwa mwanafunzi kumiliki vitu vya hatari/kifahali kama; majiko/heaters, simu,pasi ya umeme, radio, tv, deck, mavazi ya nyumbani, dhahabu na vitu vingine vya thamani, kamera, kompyuta, na vinginevyo. Vitu kama hivi huleta ubaguzi miongoni mwa walio na wasio navyo na pia huwa ni vivutio kwa wadokozi. Atakayetuhumiwa au kukamatwa navyo ataadhibiwa vikali, atanyang'anywa na vitu hivyo vitakuwa mali ya shule.*

**1.** Yampasa kila mwanafunzi atunze na kuhifadhi vizuri mali zake na mali za shule. Vifaa virudishwe mahali pake kila baada ya kazi kumalizika. Hairuhusiwi kuhamisha kifaa toka sehemu yake. Ni lazima mwanafunzi kutoa taarifa ya uharibifu au upotevu wa kifaa chochote kwa viranja. Nao viranja wafikishe taarifa hizo kwa walimu wao walezi.

**2.** Wakati wote kila mwanafunzi ahakikishe kuwa anazima taa na kufunga bomba za maji kuepuka upotevu wa nishati bure. Atakayekiuka utaratibu huu atatozwa faini ya **pesa** kufidia upotevu.

**H: WAGENI**

**1.** Mwanafunzi haruhusiwi kuonana na wageni. Wageni wote wanaofika shuleni ni wageni wa Mkuu wa Shule.

**2.** Mgeni afikapo shuleni ataelekezwa, kupokelewa na kuhudumiwa na mwalimu wa zamu kwa niaba ya Mkuu wa Shule.

**3.** Mgeni ataonesha kitambulisho chake na ataweka saini katika kitabu cha wageni wa wanafunzi. Ataeleza shida na kutoa maelezo yake kwa maandishi ambayo mwalimu wa zamu atamfikishia mwanafunzi hapo baadaye. **Ni kosa kwa mwanafunzi kutotoa taarifa kwa jamaa zake juu ya sheria hii ya wageni.**

**I: UTOAJI HABARI**

Ni kosa kubwa kupeleka taarifa, maelezo habari au barua yoyote ile kwenye vyombo vya habari bila kupitia kwa Mkuu wa Shule. Mwanafunzi haruhusiwi kupiga au kupigiwa simu. Ofisi inapokea taarifa za dharura za mwanafunzi na kumpatia haraka iwezekanavyo.

**J: TAFRIJA/ SHEREHE**

Sherehe au tafrija binafsi kama za kuzaliwa, somo wa jina, kuhitimu n.k ni marufuku hapa shuleni.

**K: KUHESHIMU, UTII NA ADABU**

*Heshima, utii na adabu ndio kielelezo cha utu wa binadamu. Ni kipimo cha kiwango cha malezi sahihi aliyopata binadamu katika makazi yake tangu utotoni. Lugha kauli na matendo ya mwanafunzi yawe yale yanayokubalika mahali popote na asilimia kubwa ya jamii na yawe yenye kuenenda na kulinda utamaduni na maadili ya Mtanzania/Mwafrika kwa ujumla. Kwa kuzingatia vema masuala ya heshima, utii na adabu ili kuepuka kujiweka matatani, kama ifuatavyo:-*

**1.** Yampasa kila mwanafunzi kuwaheshimu viranja, walimu/walezi, wageni, wenzake na wananchi kwa ujumla. Pia, aheshimu utaratibu wa sheria zote za shule na sheria za nchi hii hususani; katiba, bendera, fedha, wimbo wa taifa/shule, nembo na picha za viongozi mbalimbali. Ni wajibu wa kila mwanafunzi kusimama na kusalimia mwalimu au anayemzidi umri na kupokea mzigo mahali popote. Aidha mwanafunzi akiitwa afike haraka na pindi anapotumwa ni lazima arudishe jibu au taarifa baada ya utekelezaji wa alichotumwa.

Wanafunzi washirikiane pamoja katika kila hali ili kujenga umoja na upendo miongoni mwao bila kujali dosari au tofauti.

***2.*** Ni marufuku na ni kosa kubwa mwanafunzi kuendekeza na kujenga mahusiano binafsi kati yake na mwalimu, watumishi wengine au wana familia zao.

***3.*** Matatizo yoyote yanayohusu wanafunzi lazima yapitie ngazi zilizowekwa kuanzia viranja, walimu walezi, waandamizi na hatimaye Mkuu wa Shule. Wanafunzi wasijitwalie madaraka na mamlaka kwa kuruka ngazi na kwenda moja kwa moja ngazi za juu.

**L . Sheria na kanuni muhimu za shule.**

L.1 Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni:

a. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu.
c. Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni (preparation)
d. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
e. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
f. Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.
g. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
h. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

**L. 2 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha ukafukuzwa shule**:

a. Wizi.
b. Uasherati na ushoga.
c. Ubakaji
d. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya au kukutwa na bangi, cocaine, mirungi, kubeli, sigara n.k.
e. Kupigana au kumpiga mwanafunzi au mtumishi wa shule.
f. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
g. Kudharau Bendera ya Taifa
h. Kuoa au Kuolewa
i. Kupata mimba au kuharibu mimba ndani na nje ya shule.
j. Kulala nje ya shule bila taarifa
k. Kugoma, kuchochea na kuongoza mgomo au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
l. Kutukana watu kwa makusudi.
m. Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi au vitu vinavyohusiana na simu kama vile vocha, chaja, laini ya simu, au earphone .
n. Kukosa shule kwa siku 90 mfululizo bila taarifa rasmi.
o. Kuchelewa kufika shuleni kutoka likizo au unaporuhusiwa kutoka nje ya shule.
p. Utoro (kutoka nje ya mipaka ya shule bila ruhusa)
q .Kugomea maelekezo halali ya shule mfano kazi,chakula,masomo n.k
r. Kulala kitanda kimoja wanafunzi wawili.
s. Mwanafunzi kujihamisha bweni alilopangwa na utawala bila taarifa.

***OWM – TAMISEMI***
***HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA***

**SHULE YA SEKONDARI MSALATO**
**FOMU YA KUKUBALI SHULE**

## A. SEHEMU YA MWANAFUNZI

1. Mimi (Majina kamili) …………………………………………………………………..
   Nimekubali kuingia kidato cha …………… katika Shule ya Sekondari Msalato Dodoma kuanzia tarehe ……………… hadi nitakapomaliza kidato cha ……………
2. Naahidi kwamba nitatii sheria za Shule na kushiriki katika shughuli zote za shule kikamilifu kulingana na ratiba.
3. Tarehe ya kuzaliwa………………………..Kijiji/Mtaa………………………………….
   Tarafa…………………………………….. Wilaya ………………………………..
   Shule unakotoka ……………………………………..Namba yako ya mtihani……
4. Kituo cha gari (Bus) au Gari la Moshi kilichopo karibu na nyumbani kwako………………..
5. Nikimaliza kusoma shule ningependa kufanya kazi ifuatayo ………………………

Sahihi ya mwanafunzi ……………………. Tarehe ……………………………....

## B. SEHEMU YA MZAZI AU MLEZI

1. Mimi (majina kamili) …………………………………………………… simu……………………… ninakubali mtoto wangu asome katika Shule ya Sekondari ya Wasichana Msalato kuanzia kidato cha ………………………hadi atakapomaliza kidato cha ……………
2. Jina kamili la Mama ……………………………………………simu………………………………..
   Kazi ya Baba ………………………………………..
3. Kazi ya Mama ………………………………………
4. Anwani ya Mzazi/Mlezi …………………………….…
   …………………………………………………………
   …………………………………………………………
5. Wafuatao ni Ndugu zake ninaowatambua wanaweza kumsaidia wakati wa dharura

| Jina kamili | Mahusiano | Anakoishi | Simu yake |
|---|---|---|---|
| (i)…………………… | ……………..…… | ……………………. | …………… |
| (ii)…………………… | ……………..………. | ……………………. | …………… |
| (iii)…………………….. | ……………………… | ………………….. | …………… |

6. Madhehebu ya Dini ya Mtoto ni Lutheran/Katoliki/Anglican/PAG/TAG/ Moravian /SDA/Muislam /Nyingine

7. Ripoti zote za maendeleo ya mwanafunzi ziwe zinatumwa kwa
   ……………………………………………………..
   ……………………………………………………..
   ……………………………………………………..
   Sahihi ya Mzazi/Mlezi

   Tarehe ………………………………………………

***MSALATO SECONDARY SCHOOL***
***FORM FOR STUDENTS MEDICAL EXAMINATION***

To be completed by a Medical Officer

………………………………………….(Insert name of **the** Government Medical Institution)
Name of Student ……………………………………………. Form ………………… Year……….

Age ………………………………………………………. Sex………………………………..

Blood count ………………………………………………………………………………….

Stool …………………………………………………………………………………………

Urine …………………………………………………………………………………………

T. B. Test …………………………………………………………………………………….

Eyes ……………………………………………………………………………………………..

Ears ……………………………………………………………………………………………

Chest ……………………………………………………………………………………………..

Spleen …………………………………………………………………………………………

Abdomen ……………………………………………………………………………………

Teeth ……………………………………………………………………………………………..

Additional information:- (***e.g. pregnancy, physical defects, infections, psychological disorder, chronic or family diseases).***

……………………………………. ……………………………………………………………….

………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

**I certify that above pupil is fit to continue with studies in Secondary School for four years.**

Name of Medical Officer ………………………………………………Signature ……………………

Designation …………………………………..

Station & Official Stamp………………………………….. Date ………………………….

***A student must undergo a thorough medical check up before the form to be filled in by a doctor. For any cheating case, strong measures shall be taken upon a responsible student including the doctor who has filled in the form since it is against human rights.***